**MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO YA HALMASHAURI TAREHE 30-31/08/2018**

**Mahudhurio**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. | Kashunju S.R | Mwenyekiti |
| 2. | Mh. | Jonas T. Vedasto | Mjumbe |
| 3. | Mh. | Theophila K. Theobard | Mjumbe |
| 4. | Mh. | Henery F. Bashasha | Mjumbe |
| 5. | Mh. | Gaspary B. Gabriel | Mjumbe |
| 6. | Mh. | Hasanat M. Chamani | Mjumbe |
| 7. | Mh. | Devotha Nestory | Mjumbe |
| 8. | Mh. | Hyasintha T. Katita | Mjumbe |
| 9. | Mh. | Restuta K. Kafuba | Mjumbe |
| 10. | Mh. | Sevelini P. Bugoha | Mjumbe |
| 11. | Mh. | Byarufu R. Beneth | Mjumbe |
| 12. | Mh. | Benan L. Rwabalema | Mjumbe |
| 13. | Mh. | Ernest Kalisa | Mjumbe |
| 14. | Mh. | Angelo G. Rwaibebe | Mjumbe |
| 15. | Mh. | Fulgence M. Frederick | Mjumbe |
| 16. | Mh. | Bahati Henericko | Mjumbe |
| 17. | Mh. | Consolatha Kanyima | Mjumbe |
| 18. | Mh. | Daud S. Mashurano | Mjumbe |
| 19. | Mh. | Prudence Mweyunge | Mjumbe |
| 20. | Mh. | Joel S. Nshobeilwe | Mjumbe |
| 21. | Mh. | Emmanuel N. Alfred | Mjumbe |
| 22. | Mh. | Jovinary K. John | Mjumbe |
| 23. | Mh. | Devotha M. Byashara | Mjumbe |
| 24. | Mh. | Joyleth G. Mutashaga | Mjumbe |
| 25. | Mh. | Clepin R. Bernard | Mjumbe |
| 26. | Mh. | Eustace L. Christian | Mjumbe |
| 27. | Mh. | Laurean M. Simon | Mjumbe |
| 28. | Mh. | Kimalala G. Eustace | Mjumbe |
| 29. | Mh. | Majaliwa John | Mjumbe |
| 30 | Mh. | Said Abdunuru | Mjumbe |
| 31. | Ndg. | Shadrack M. Mhagama | Katibu |

**Wataalam:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mayala P. Sengerema | Kny:Mkuu wa idara ya elimu msingi na sekondari |
| 2. | Eliah Shedehwa | Kaimu AfisaTarafa Murongo |
| 3. | Meshack Libenti | Mkuu wa idara ya kilimo, ushirika na umwagiliaji |
| 4. | Juma Magotto | Mkuu wa idara ya Ujenzi na zimamoto |
| 5. | Nassoro Ngulungu | Mkuu wa kitengo cha ukaguzi wa ndani |



Scanned by CamScanner

6. Prosper Rutakinikwa — Kaimu mkuu wa idara ya mifugo na uvuvi
7. Fredinand Tindamanyire — Mkuu wa idara ya maji
8. G.L. Rugaimukamu — Afisa Tarafa Kaisho
9. Revocatus Josephat — Mkuu wa idara ya maendeleo ya jamii, ustawi wa jamii na vijana
10. Deusdedith Bagenyi — Dereva
11. David Augustine — Dereva
12. Evarista Chacky — Afisa usafirishaji
13. Lazaro Majeta — Kaimu mkuu wa kitengo cha uchaguzi
14. Frolent Bugingo — Kny:Mkuu wa idara ya mipango, takwimu na ufuatiliaji
15. Richard Mayiku — Kaimu mkuu wa idara ya ardhi na maliasili
16. Thomas A. Mahenge — Kaimu mkuu wa kitengo cha nyuki
17. Yassin Juma. — Afisa uvuvi
18. Alex Kaganda — Mkuu wa kitengo cha manunuzi ya umma na ugavi
19. Dr. Diocles Ngaiza — Kaimu mganga mkuu wa Wilaya
20. Debora Ngangaji — Mkuu wa idara ya utawala na utumishi
21. Musa A. Jumanne — Afisa Tarafa Mabira
22. Melchades Colonely — Kny: Mkuu wa idara ya fedha na biashara
23. Emmanuel Lyanga — Mratibu wa TASAF III
24. Obed Kamwela — Mdhibiti kahawa
25. Golden Nzalalila — Mratibu maafa
26. Jonathani Kikasiga — Afisa ushirika
27. Joanitha Balthazari — Afisa utumishi
28. Alexander Lundera — Kaimu mkuu wa kitengo cha TEHAMAU
29. M.Z.Mutafungwa — Afisa Tarafa Nkwenda
30. Memory J. Mapunda — Afisa vijana

**Waalikwa:**

1. Rashid Mohamed Mwaimu — Mkuu wa Wilaya
2. Greyson I. Mwengu — Katibu tawala wa Wilaya
3. CAPT. AD Ndelwa — Mshauri wa mgambo wa Wilaya
4. Rachel Mkama — Mwandishi FADEKO radio
5. Ezra Rugakila — Mwandishi Radio Karagwe
6. SP Justin E. Joseph — Mkuu wa polisi wa Wilaya
7. Elias Joseph — Afisa usalama
8. Nuhu Badiru — Shekh wa Wilaya
9. Rev. Pius Peter — Mchungaji
10. 2LT EF Konga — DET COM- Kaisho
11. SISGT. Peter Mmbare — Kamanda zimamoto
12. Fratha Katumwa — Katibu wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya
13. Bazil Waziri — Katibu Chama cha Demokrasia na Maendeleo Wilaya
14. Kenneth Rugumila — Kaimu meneja TARURA
15. Wilson Mwapwele — Mkuu wa TAKUKURU Kyerwa



Scanned by CamScanner

16. Kamaliza Julius — Mwandishi radio Kwizela
17. ASP G.Kyekaka — Afisa Magereza
18. Innocent Mumburi — Afisa uhamiaji Kyerwa
19. Martin Rutasyamuka — Mwenyekiti wazee Wilaya
20. Daniel Damian — Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya

**Sekretarieti:**

Ildephonce Valentine
Asimwe Henery

**Agenda:**

**SIKU YA KWANZA ALHAMISI, TAREHE 30/08/2018**

1. Taarifa ya Mwenyekiti wa Halmashauri akifungua rasmi mkutano wa Baraza la madiwani Agosti, 30 – 31/8/2018
2. Kuthibitisha dondoo
3. Maelekezo ya Serikali
4. Maswali ya papo kwa papo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya
5. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 28-29/06/2018
6. Utekelezaji wa maazimio kikao kilichopita cha tarehe 28-29/06/2018
7. Kupokea taarifa ya utendaji wa uwajibikaji wa Halmashauri kutoka kwa Wenyeviti wa kamati za kudumu kwa kipindi cha robo ya nne 2017/2018
   i) Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango
   ii) Kamati ya Elimu, Afya na Maji
   iii) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
   iv) Kamati ya kudhibiti UKIMWI
8. Taarifa za Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya
   i) Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018
   ii) Taarifa ya ukaguzi wa ndani kwa mwaka wa fedha 2017/2018
   iii) Taarifa ya manunuzi na Bodi ya zabuni kuanzia Julai, 2017 hadi Juni, 2018
   iv) Mpango wa motisha kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa
   v) Taarifa ya Kitengo cha sheria kwa kipindi cha robo ya nne kuanzia Aprili hadi Juni, 2018
   vi) Kupitisha na kuidhinishwa sheria ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa
   vii) Taarifa juu ya mpango wa usimamizi shirikishi na sheria ndogo ya msitu wa hifadhi MTAGATA

**SIKU YA PILI IJUMAA, TAREHE 31/08/2018**

9. Kujadili taarifa ya utendaji na uwajibikaji wa Halmashauri kwa mwaka 2017/2018
10. Kumchagua Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri
11. Kuteua wajumbe wa Kamati za kudumu
12. Kupitisha ratiba ya vikao vya kisheria vya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa mwaka wa fedha 2018/2019
13. Kufunga kikao



Scanned by CamScanner

**KU/KYR/BM/30/2017/2018 KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alieleza kuwa ni mkutano wa kawaida kwa robo ya nne 2017/2018. Alisema kuwa kabla ya kufungua litafanyika zoezi la kuapisha Waheshimiwa Madiwani wawili wa kata ya Kibare na Bugomora. Ulifanyika utambulisho katika nyanja zote. Alimkaribisha mwenyekiti kufungua kikao, Mwenyekiti aliwakaribisha waheshimiwa madiwani wapya wa kata za Kibare na Bugomora. Katika hotuba yake alimkaribisha na kumpongeza Mh. Rashid Mohamed Mwaimu kuteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa.

Alieleza kwamba wananchi na viongozi kwa ujumla wafanye kazi kwa ushirikiano. Alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kutoa fedha ya miradi ya maendeleo Tsh. bilioni 1.5. Pia alisema kuwa mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya Murongo umekamilika kwa 98%. Alipongezwa Mkurugenzi na timu yake kusimamia miradi hasa kituo cha afya Murongo. Zimepokelewa Tsh. milioni 400 katika kituo cha afya Kamuli na kusisitiza kusimamia vizuri mradi huo.

Umefungwa Mfumo wa kudhibiti mapato katika vituo vya afya, katika wilaya ya Kyerwa wameishaanza kufungua mfumo huo kwenye vituo vya afya vya Murongo na Nkwenda.

Aliwaomba wazazi kuwaruhusu wanafunzi wakati wa kufanya mtihani wa kumaliza darasa la saba kuhudhuria ipasavyo.

Sekta ya maji inatekeleza mradi wa maji katika vyanzo vya maji Isingiro, makao makuu mradi umekamilika na kutoa huduma, vifaa vilivyochakaa viondolewe. Vyanzo vya maji ambavyo havifanyi kazi vifufuliwe na kuanza kufanya kazi na kudhibiti vyanzo vya maji visivamiwe.

Sekta ya kilimo, aliwashukuru wakulima na kuomba walipwe pesa zao baada ya kuuza kahawa.

Kuhusu Mapato ya ndani kwa kipindi hiki hawakukusanya vizuri kwa sababu mapato yanayotokana na kahawa hayajatolewa. Halmashauri imefikia 78% sababu kahawa ilikuwa haijauzwa.

Sekta ya uvuvi, Halmashauri ina rasilimali nyingi kama samaki inayotumika kama kitoweo na kuomba kuhamasisha wadau mbalimbali kufuga samaki.

Uchomaji moto, ilielezwa kuwa kuna tatizo la uchomaji moto hivyo ilisisitizwa kulikemea ili lisijitokeze tena.

Baada ya kusema hayo alifungua kikao rasmi mnamo saa 6:02 mchana.

Ilitolewa nafasi kwa Meneja 'TANESCO' kutoa ufafanuzi juu ya masuala ya umeme.

Meneja alieleza kuwa mradi wa 'REA' awamu ya pili umemalizika na alisema kwamba inaandaliwa ofisi rasmi ya Wilaya. Baadhi ya watu ambao hawajaunganishiwa umeme wataunganishiwa kabla ya mkataba kufungwa. 'Mradi wa REA' awamu ya tatu kazi ya utafiti imemalizika kwenye vijiji 21 na mkandarasi yupo eneo la kazi zoezi litaanza mara moja.



Scanned by CamScanner

Ilielezwa kuwa kuna changamoto ya uchomaji moto iliyosababisha kuunguza nguzo za umeme 48 na kusababisha hasara kubwa kwenye shirika.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walihoji kama ifuatavyo:-

**Hoja**: Lini waliolipia umeme kata ya Rutunguru awamu ya kwanza watapewa umeme?

**Ufafanuzi**: Mkataba ulishafungwa na tatizo la kutokamilisha ni kuishiwa vifaa lakini suala hilo litafanyiwa kazi.

**Hoja:** Kata Businde ipo kwenye mpango wa kupatiwa umeme awamu ya tatu?

**Ufafanuzi**: Kata Businde ipo kwenye mpango na itapatiwa umeme.

**Hoja**: Kwa nini umeme unakatwa mara kwa mara?

**Ufafanuzi**: Wanaokata umeme ni wanaotuuzia umeme ambao tunaununua Uganda.

**Hoja**: Lini Taasisi zitapatiwa umeme ikiwemo zahanati ya Rwabwere?

**Ufafanuzi**: Taratibu zilishafanyika lililopo ni kufanya 'wiring' baada ya taratibu kukamilika umeme utawekwa.

**Hoja**: Lini watumishi waliopo makao makuu ya wilaya watapatiwa umeme?

**Ufafanuzi**: Kipindi cha kufanya utafiti nyumba zilikuwa hazijajengwa lakini wateja watawekwa kwenye mpango na kufikia mwezi Novemba 2018 wanaweza kupatiwa umeme.

**KDCU**

Meneja, alieleza kwamba zoezi la ukusanyaji kahawa kwa wakulima linaenda vizuri. Baadhi ya wakulima walilipwa fedha zao na wengine bado ambao bado watapatiwa baada ya fedha kutolewa.

**Hoja**: Kwa nini haijatajwa bei ya kuuza?

**Ufafanuzi**: Bei ya kuuza inajulikana baada ya mnada isipokuwa waliouza mwezi Julai itaongezwa Tsh. 400 na itabadilika kadiri ya bei ya mnada utakavyokuwa.

**Hoja**: Kwa nini karani hawatoi stakabadhi kwa wakulima baada ya kuuza kahawa na kusafirisha fedha bila ulinzi?

**Ufafanuzi**: Suala la kutopewa stakabadhi na kusafirisha fedha bila ulinzi litafanyiwa kazi.

**KU/KYR/BM/31/2017/2018 TAARIFA YA SERIKALI**

Mkuu wa Wilaya alimshukuru Mh, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa. Alieleza kuwa ameletwa Wilaya ya Kyerwa kusimamia na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Pia alieleza kuwa lazima kusimamia mapato ya



Scanned by CamScanner

Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ili kuweza kujipatia maendeleo. Ilishauriwa kubuni vyanzo vingine vya mapato ili kuweza kuongeza mapato.

Matumizi yote ya fedha za Serikali yatumike kwa usahihi kulingana na thamani ya fedha inayotolewa. Pia miradi yote ya maendeleo itekelezwe kwa uweledi. Ulitolewa ushauri kwa vijana kupatiwa maeneo ya kufanya ujasiliamali wao na kuanzisha vikundi vya ujasiliamali.

Kuhusu kahawa, alieleza kuwa kahawa ipelekwe kwenye vyama vya msingi na siyo kupelekwa nchi jirani ya Uganda.

**Azimio, Zilitolewa siku 10 kuanzia tarehe ya kikao hiki kila mkulima apeleke kahawa kwenye vyama vya msingi.**

**Azimio, Makarani wanaolipa wakulima kwa upendeleo wakamatwe na kuchukuliwa hatua.**

Zitolewe stakabadhi kwa wakulima wanaouza kahawa kwenye vyama vya msingi. Pia biashara ya butura ikomeshwe haraka iwezekanavyo.

**Azimio, Vianzishwe vikoba/SACCOS kwenye vijiji na kuhakikisha elimu inatolewa na kuanza kufanya kazi.**

Miundombinu ya umeme inapaswa kulindwa kwa nguvu zote ili kuepusha hasara zinazojitokeza kwa kuchoma moto na kuunguza nguzo za umeme.

Kamati za moto kwenye vijiji, kata na vitongoji ziwajibike kudhibiti moto na moto ukiwashwa kamati hizo ziwajibishwe.

Zitatuliwe changamoto za wananchi katika sekta ya afya, maji, elimu na barabara kwa wakati ili kupata huduma iliyo bora.

Alieleza kwamba hifadhi ya Ibanda Rumanyika Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameridhia kuwa hifadhi ya Taifa. Hivyo alisisitiza kuweka mazingira ya kuwapokea wageni katika namna ya kuwahifadhi na kuwahudumia.

Alisisitiza wafanyakazi wa umma kufanya kazi kwa bidii na kuacha tabia ya kufanya kazi kwa mazoea.

Lilitolewa tangazo na mkuu wa wilaya kuwa ichukuliwe tahadhari kwa wananchi hasa kwenye mpaka wa Murongo katika suala la ugonjwa wa ebora.

**Azimio, Iwepo rejista kwa kila idara namna ya kupokea na kutoa huduma kwa wananchi.**

**Azimio, Kila idara lazima kuwepo na "morning prayer" na kufanya tathmini ya utendaji kwa kila siku.**

**KU/KYR/BM/32/2017/2018 MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

**Mh Angelo Rwaibebe**



Scanned by CamScanner

**Swali,** Ni lini barabara ya Isingiro - Nyabishenge - Rwamashaju itakamilika?

**Jibu**, Zilitolewa fedha kidogo na fedha nyingine zikipatikana itakamilika.

**Mh Sevelin Bugoha**

**Swali**, Kuna mkakati gani wa kuweka maji kituo cha afya Murongo?

**Jibu**, Wanaoendelea na mradi wa umeme walikubaliana kupeleka maji kituo cha Afya Murongo na chanzo cha maji kimeishatambuliwa hivyo maji yatawekwa.

**Mh Laurian Magezi**

**Swali**, Kuna mpango gani wa kuanzisha shule makao makuu ya Wilaya ya Kyerwa?

**Jibu**, Ujenzi wa shule, lazima kutolewa taarifa mapema ili kuweza kuwekwa kwenye bajeti.

**Mh Fulgence Frederick**

**Swali**, Wananchi waliotolewa eneo la magereza ni lini watalipwa fidia zao?

**Jibu**, Suala la fidia lipo kwa Kamishina wa Magereza majibu yakitolewa wananchi watajulishwa na kulipwa fidia yao.

**Mh Christian Eustace**

**Swali**, Ni lini shule ya msingi Mukunyu itapatiwa walimu wa kutosha?

**Jibu**, Serikali inaendelea kuleta walimu na wanaofika wanapangiwa vituo vyenye uhitaji wa walimu lakini awamu hii kata ya Kikukuru walipelekwa walimu 4.

**Mh Clepin Bernad**

**Swali**, Barabara ya Nyarutuntu kwenda Rushanje lini mradi utakamilika?

**Jibu**, Fedha ikipatikana barabara zitakamilishwa.

**Mh Devotha Byashara**

**Swali**, Lini ofisi za Halmashauri zitakamilika?

**Jibu**, Ujenzi unaendelea baada ya kufunga mkataba na SUMA JKT na malipo ya awali Tsh. Milioni 150 zitalipwa baada ya mtandao kukaa vizuri.

**Mh, Henery Bashasha**

**Swali**, Ni lini shule mpya ya msingi Ihanda itatembelewa ili kuruhusu kufunguliwa?

**Jibu**, Shule itatembelewa kama inakidhi vigezo itafunguliwa.



Scanned by CamScanner

**Mh, Bahati Henerico**

**Swali**, Kuna barabara ambazo hazina Kalvati ni lini kalvati zitawekewa?

**Jibu**, Fedha ikipatikana zitajengwa kalvati inapobidi.

**Mh, Majaliwa Mapambano**

**Swali**, Lini wodi ya wazazi katika kituo cha afya Nkwenda itaanza kufanya kazi?

**Jibu**, Zikipatikana fedha ujenzi utakamilika.

**Mh, Tulakila Twijuke**

**Swali**, Lini jengo la zahanati ya Nyamiyaga litakaguliwa na kuruhusu kuanza kufanya kazi?

**Jibu**, Litafanyiwa kazi

**Mh, Beneth Byarufu**

**Swali**, Lini mhandisi wa ujenzi atafika shule mpya ya Chakarisa ili kuruhusu ujenzi?

**Jibu**, Shule itatembelewa.

**Mh, Hyasinta Katita**

**Swali**, Lini shule ya kidato cha sita itaanza Wilaya ya Kyerwa?

**Jibu**, Taratibu zinaendelea za kuanzisha shule ya kidato cha tano na sita katika shule ya sekondari Nyabishenge na Mabira. Fedha ikipatikana itaanza shule ya sekondari Mabira.

**Mh, Jovinary John**

**Swali**, Lini mradi wa maji utakamilika uliopo Chanyangabwa na Songambele?

**Jibu**, Wakandarasi watakamilisha miradi yao baada ya fedha za wakandarasi kulipwa.

**Mh, Ernest Kalisa**

**Swali**, Lini mradi wa stendi na soko la Isingiro itaanza kufanya kazi?

**Jibu**, Mkataba umeishafungwa stendi ya Nkwenda na Isingiro itaanza muda mfupi.

**Mh, Hasanath Chamani**

**Swali**, Halmashauri imejipangaje kuwezesha wanyeviti wa vijiji?

**Jibu**, Ufanyike usimamizi wa mapato fedha ikipatikana watalipwa kwa 20% itakayorudishwa.



Scanned by CamScanner

**Mh, Gaspari Gabriely**

**Swali**, Lini watapatikana waganga kwenye zahanati ya Mugaba inayotumiwa na kata mbili ya Businde na Bugara?

**Jibu**, Serikali ikitoa ajira watapelekwa waganga katika zahanati hiyo.

**Mh, Restuta Kafuba**

**Swali**, Lini mradi wa maji Kigorogoro utakamilika ili wananchi waweze kupata maji?

**Jibu**, Zoezi la ukamilishaji mradi linaendelea, sasa hivi yananunuliwa mafuta kwa ajili ya kusambaza maji kwa wananchi.

**KU/KYR/BM/33/2017/2018 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 28-29/06/2018**

Muhtasari ulisomwa na kufanyiwa masahihisho kuwa ukurasa wa sita neno uhamaishaji kuandikwa uhamasishaji. Baada ya masahihisho muhtasari ulisainiwa na kuwa kumbukumbu halali.

**KU/KYR/BM/34/2017/2018 UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 28-29/06/2018**

**Hoja:** Maafisa tarafa wahakikishe vijana wanafanya kazi na kila kijana zaidi ya miaka 18 aonyeshe shamba lake. Pia kila kaya kuhakikisha ina bustani/miti ya matunda isiyopungua 5.

**Utekelezaji**: Agizo limetekelezwa barua yenye kumb. Na BA.926/23/03/37 ya tarehe 15/07/2018. Iliandikwa kwa Maafisa tarafa na nakala kwa Watendaji wa kata na Maafisa kilimo kwa utekelezaji. Katika barua hii waliagizwa kuhamasisha vijana kufanya kazi. Pia kila kaya kupanda miche ya matunda isiyopungua 5. Aidha barua iliagiza zoezi la ukaguzi kuanza 30/08/2018.

**Hoja**: Kamati zote za moto zihakikishe moto ukiwashwa lazima kuuzima ikishindikana viongozi wote wawajibishwe.

**Utekelezaji**: Watendaji wa Kata waliandikiwa barua yenye Kumb.Na.FB.605/974/20/13 ya tarehe 17/07/2018 ikiwataka kudhibiti uchomaji moto katika maeneo yao, barua hiyo ilitumwa kwa Maafisa tarafa.

**Hoja**: Yatolewe maelezo kwa maandishi kujengwa shule ya msingi Rulama chini ya kiwango na wahusika wakamatwe.

**Utekelezaji**: Ukaguzi ulifanyika na kuchukua hatua za kurekebisha kasoro zilizojitokeza kwa ushirikiano wa walimu na kamati ya shule. Hatua za wahusika kukamatwa zilihairishwa ili ushirikiano uendelee. Ni pamoja na kuleta mbao na mabati kwa kutumia kiasi cha fedha zilizopo.



Scanned by CamScanner

**Hoja**: Zipelekwe sheria ndogo za Halmashauri kwenye kata na kuanza kufanya mchakato kwenye kata

**Utekelezaji:** Watendaji wa kata wote walipatiwa rasimu za sheria ndogo na wameanza kuleta maoni.

Ilihojiwa kwamba sheria ndogo zilizotumwa kwenye kata hazikuletwa katika kata ya Kitwe. Ilijibiwa kwamba sheria zote zilipelekwa kwenye kata kwa barua.

**Hoja:** Yawasilishwe maombi ili mtendaji wa kata aliyekuwa kata ya Businde aje kukabidhi Ofisi

**Utekelezaji:** Mtumishi Colnery C.Kijwala alishakamatwa kwa ushirikiano wa ofisi na Jeshi la polisi na suala lake bado liko polisi kwa hatua ya upelelezi.

**KU/KYR/BM/35/2017/2018 KUPOKEA TAARIFA YA UTENDAJI WA UWAJIBIKAJI WA HALMASHAURI KUTOKA KWA WENYEVITI WA KAMATI ZA KUDUMU KWA KIPINDI CHA ROBO YA NNE 2017/2018**

**Kamati ya fedha, uongozi na mpango**

Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.

**Kamati ya elimu, afya na maji**

Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-

**Hoja**: Ni lini mradi wa maji Isingiro utarekebishwa ili wananchi waweze kupata maji?

**Jibu**, Fedha ya kumlipa mkandarasi bado haijalipwa akilipwa ataendelea na kazi ili kukamilisha mradi.

**Hoja**: Kwa nini walengwa wa TASAF III wenye uwezo wanapewa fedha?

**Jibu**, Wabainishwe wenye uwezo na kuondolewa kwenye mpango wa TASAF III hasa mgombea wa udiwani kata Kibare.

**Kamati ya Ujenzi, Uchumi na Mazingira**

Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-

**Hoja**: Lini mgogoro wa ardhi ya Kaitambuzi utatatuliwa?

**Jibu**: Mgogoro ulishughulikiwa mara 5 lakini haukupata suruhu. Tarehe iliyopangwa suala hili litafanyiwa kazi.

**Kamati ya kudhibiti UKIMWI**

Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.



Scanned by CamScanner

**KU/KYR/BM/36/2017/2018 TAARIFA ZA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA**

**i. Miradi ya Maendeleo**

Taarifa iliwasilishwa na wajumbe kuhoji kama ifuatavyo:-

**Hoja**: Kwa nini miradi ambayo haijakamilika isikamilishwe kwa wakati hasa shule ya msingi Omukiyonza?

**Ufafanuzi:** Miradi itakamilishwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Taarifa ilipokelewa.

**ii. Taarifa ya mkaguzi wa ndani**

Taarifa ilipokelewa.

**iii. Taarifa ya manunuzi na Bodi ya zabuni.**

Taarifa ilipokelewa.

**iv. Taarifa za sheria ndogo za Halmashauri**

Ulitolewa ushauri wa kupaka rangi nyumba zenye mpango mji ambao ni Isingiro, Mabira, Murongo na Kyerwa.

Taarifa ilipokelewa na kuruhusu kuendelea na hatua nyingine.

**SIKU YA PILI TAREHE 31/8/2018**

**KU/KYR/BM/37/2017/2018 KUJADILI TAARIFA YA UTENDAJI NA UWAJIBIKAJI WA HALMASHAURI KWA MWAKA 2017/2018**

Iliwasilishwa taarifa kama ifuatavyo:-

Halmashauri ya wilaya ya Kyerwa imetekeleza majukumu yake mbalimbali kama ifuatavyo:- Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 28 katika shule za msingi 15, Vyumba 17 kati ya 28 vimekamilika, Vyumba 11 vipo hatua tofauti ya ukamilishaji.

Ukamilishaji wa matundu ya vyoo 56 katika shule 12 za msingi Matundu ya vyoo 56 yamekamilika na yanatumika.

Ukamilishaji wa vyumba 18 vya madarasa katika shule 05 za Sekondari Vyumba 15 kati ya 18 vimekamilika, Vyumba 03 vipo hatua tofauti ya ukamilishaji.



Scanned by CamScanner

Ukamilishaji wa Maabara 03 za masomo ya Fizikia, Kemia, na Biologia katika shule za Sekondari za Kyerwa na Murongo.

Kuongezewa mtaji/Kuongeza vifaa katika vikundi vya akina mama

- Vikundi 03 vimesaidiwa kiasi cha fedha Tsh.1,000,000.00 kila kimoja

Kaya maskini sana 7980 zinaendelea kupokea ruzuku na kugharamia mahitaji muhimu kama chakula, mavazi na malazi. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2017 jumla ya Tsh. **1,662,136,000** zimetolewa na walengwa.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walihoji kama ifuatavyo:-

**Hoja**: Lini vijiji ambavyo havipo kwenye mpango wa TASAF III vitaingizwa kwenye mpango?

**Ufafanuzi**: Ni kusubiri taratibu kutoka makao makuu TASAF III wakiruhusu vijiji vilivyobaki vitaingizwa.

**Hoja:** Lilitolewa ombi la kumalizia miradi ambayo haijakamilika. Ulitolewa ushauri wa kumalizia majengo yaliyopo kwenye hatua nzuri kwa kiasi kinachopatikana.

**Ufafanuzi:** Miradi inatekelezwa kwa kuzingatia bajeti hivyo miradi ambayo haijakamilika itakamilishwa baada ya fedha kupatikana.

Aliombwa Mkuu wa Wilaya kufuatilia suala la kahawa na kuhakikisha wakulima wanapata fedha yao mapema. Pia ulitolewa ushauri wa kufufua SACCOS na kuendeleza zao la vanilla katika wilaya ya Kyerwa.

Ilishauriwa uwekwe utaratibu mzuri wa kuuza mafuta ya petrol kwenye vibanda/maduka ili kuepusha hatari ya moto.Taarifa ilipokelewa.

**KU/KYR/BM/38/2017/2018 KUTEUA WAJUMBE WA KAMATI ZA KUDUMU**

I. **Kamati ya ujenzi, uchumi na mazingira**

1. Mh. Kimalala G. Eustace
2. Mh. Consolatha Kanyima
3. Mh. Eustace R. Christian
4. Mh. Said A. Mukandara
5. Mh. Jovinary K. John
6. Mh. Emmanuel N. Alfred
7. Mh. Prudence Mweyunge
8. Mh. Sadath Jeremiah
9. Mh. Benan L. Rwabalema
10. Mh. Restuta K. Kafuba
11. Mh. Fulgence M. Frederick
12. Mh. Hyasinta Katita



Scanned by CamScanner

13. Mh. Kashunju S.R (Mwenyekiti)
14. Mh. Sevelini Bugoha
15. Mh. Bahati Henerico
16. Mh. Devotha Byashara
17. Mh. Beneth A. Byarufu
18. Mh. Joel Nshobeirwe

Wagombea nafasi ya Mwenyekiti wa kamati ni:-

1. Fulgence Frederick alipata kura 10
2. Benani Rwabalema alipata kura 7

Hivyo mwenyekiti wa kamati ya ujenzi, uchumi na mazingira ni Mh, Fulgence Frederick.

**II. Kamati ya elimu, afya na maji**

1. Mh. Clepin R. Bernard
2. Mh. Kashunju S.R (Mwenyekiti)
3. Mh. Laurean Magezi
4. Mh. Joyleth G. Mutashaga
5. Mh. Henery F. Bashasha
6. Mh. Daud S. Mashurano
7. Mh. Gaspari B. Gabriel
8. Mh. Majaliwa John
9. Mh. Theofila K.Theobard
10. Mh. Ernest Kalisa
11. Mh. Tulakira Twijuke
12. Mh. Devotha N. Ikambuza
13. Mh. Hasanath M. Chamani
14. Mh. Angelo Rwaibebe
15. Mh. Jonas Vedasto

Wagombea nafasi ya Mwenyekiti ni:-

i. Henery bashasha 7
ii. Ernest Kalisa 8

Hivyo mwenyekiti wa kamati ya elimu, afya na maji ni Mh, Ernest Kalisa

**KU/KYR/BM/32/2017/2018 KUMCHAGUA MAKAMU WA MWENYEKITI WA HALMASHAURI**

**Kura zilizopigwa 31**

1. Jonas Vedasto Kura alizopata ni 17
2. Emmanuel Alfred kura alizopata ni 14



Scanned by CamScanner

Alitangazwa Mh, Jonas Vedasto kuwa makamu mwenyekiti wa Halmashauri.

**KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI**

1. Mh. Jonas T. Vedasto
2. Mh. Kashunju S.R (Mwenyekiti)
3. Mh. Bahath Henerico
4. Mh. Innocent Bilakwate (Mbunge)
5. Mh. Clepin R. Bernard
6. Mh. Devotha Byashara
7. Mh. Theofila Theobard

**KAMATI YA MAADILI**

1. Mh. Beneth R. Byarufu (Mwenyekiti)
2. Mh. Hasanath Chamani
3. Mh. Angelo Rwaibebe
4. Mh. Henery F. Bashasha
5. Mh. Joyleth Mtashaga

**KAMATI YA ALAT**

1. Mh. Devotha Byashara
2. Mh. Bahati Henerico

**KAMATI YA ARDHI**

1. Mh. Restutha Kafuba
2. Mh. Joel Nshobeilwe

**MFUKO WA JIMBO**

1. Mh. Clepin R. Bernard
2. Mh. Hasanath Chamani

**KAMATI NDOGO YA MABORESHO (TUH)**

1. Mh. Bahati Henerico
2. Mh. Gaspary Gabriely
3. Mh. Kashunju S.R

**BODI YA AJIRA**

1. Mh. Sevelini P. Bugoha

**KU/KYR/BM/39/2017/2018 KUPITISHA MAPENDEKEZO RATIBA YA VIKAO VYA KISHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

Ratiba ilipitishwa kuendelea na taratibu kwa mwaka wa fedha 2018/2019.



Scanned by CamScanner

**KU/KYR/BM/40/2017/2018 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiano mzuri na kuwapongeza wajumbe waliochaguliwa makamu mwenyekiti pamoja na wenyeviti wa kamati za kudumu. Pia ilipongezwa timu ya menejimenti kwa usimamizi mzuri wa shughuli mbalimbali kwenye Halmashauri. Alisisitiza kutekelezwa maagizo yote yaliyotolewa. Baada ya kusema hayo alifunga mkutano/kikao mnamo saa 8:58 mchana.

Saini………………………………

Jina SHADRACK M. MHAGAMA

Katibu

Saini…………………………

Jina KASHUNJU S. R

Mwenyekiti

Tarehe 31.12.2018

Scanned by CamScanner